**Hati ya Kuhitimu Kisomo cha Sekondari**

**KISWAHILI**

**Karatasi ya 3**

**FASIHI**

**Muda: Saa 2½**

## SEHEMU A

**1. Fafanua ufaafu wa anwani 'Chozi la Heri' (al. 20)**

- Mwandishi antueleza kuwa Ridha alipokwenda shuleni siku ya kwanza alitengwa na wenzake kwani hawakutaka ashiriki michezo yoa. Kijana mmoja mchokozi alimwita 'mfuata mvua' aliyekuja kuwashinda katika mitihani yote. Ridhaa alifululiza nyumbani na kujitupa mchangani na kulia kwa kite na shake. Mamake alimliwaza na kumhakikishia kumwona mwalimu keshoye. Tagnu siku hii, hu ukawa ndio mwanzo wa maisha ya heri kwa Ridhaa kwani baada ya mwalimu kuzungumza na wanafunzi umuhimu wa kuishi pamoja kwa kufikia kilele cha elimu ni kuhitimu kama daktari.
- Ridhaa alipotoka kwenye msitu wa mamba alijiona nafuu kwani wapwa zake – Lime na Mwanaheri walikuwa wamepata matibabu. Dadake Subira alitibiwa akapona. Mwamu wake kaizari amepona donda lililosababishwa na kutazama mabinti zake wakitendewa ukatili (kukabwa) na vijana wenzao. Ridhaa anajua kuwa Kaizari ni afadhali kwa sababu hakuna aliyemtenga na mmoja kati ya jamaa zake. Ridhaa anapomfiira Kaizari anajiambia heri nusu shari kuliko shari kamili.
- Ridhaa aliposikia sauti ya kike ikitangaza, tangazo lile lilimrudisha katika mandhari yake ya sasa. Alijaribu kuangaza macho yake aone anakoenda lakini macho yalijaa na kutiririka yatakavyo.
- Wakati Ridhaa alimkazia macho Mwangeka alikuwa akijiuliza iwapo babake amekuwa mwehu kwa kukosa kushirikiana na majiriani kuchimba kaburi kuyazika majivu – matone mazito ya machozi yalitunga machoni mwake Mwangeka. Akayaacha yamdondoke na kuchiririza yatakavyo. Uvuguvugu ulitokawa na mwanguko wa machozi wa machozi haya uliulainisha moyo wake, ukampa amani kidogo. Moyo wake ukajaa utulivu kwa kujua wino wa Mungu haufitiki.
- Wakati Ridhaa alikuwa akisimulia Mwangeka misiba iliyomwandama tangu siku alipoondoka kwenda kuweka amani Mashariki ya kati, Ridhaa alisita akajipangusa kijasho kilichokuwa kimetunga kipajini mwake kisha akatoa kitambaa mfukoni na kuyafuta machozi yaliyokuwa yameanza kumpofusha.
- Mwangeko alipokuwa ameketi mkabala na kudimbwi cha kuogolea, mawazo yake yalikuwa mbali alikoanzia akawa anakumbuka changamoto za ukuaji wake. Akawakumbuka annatola (Tila) mwilo ulimzizima kidogo akatabasamu kisha tone moto la chozi likamdondoka.

- Katika msitu wa samba kulikuwa na maelfu ya watu waliogura makwao. Kati ya familia zilizoguria humu ni familia ya bwana Kangata. Kwa Kangata na mkewe. Ndevine hapa palikuwa afadhali kwani hawakuw na pa kwenda kwa kuwa hata kule walikokuwa wakiishi awali hakukuwa kwao.
- Wakati Dick walikutana kisadfa na Umu katika uwanja wa ndege, walikumbatiana kwa furaha. Machozi yaliwadondoka wote wawili na wakawa wanalia kimyakimya. Walijua fika kuwa jaala ilikuwa imewakutanisha na kwamba hawatawalu kutengana tena. Maisha sasa yalianza kuwa ya heri kwao.
- Baada ya miaka kumi ya kuuza dawa za kulevya, Dick alifaulu hatimaye kujinasua kutoka kwa kcha za mwajiri wake. Alianza biashara yake mwenyewe ya kuuza vifaa vya umeme. Sasa akaanza kijitegemea kwa kuwa amejiajiri. Alikuwa amefungua ukurasa mpya katika maisha yake. Maisha yake sasa ni ya heri.
- Wakati Neema na Mwangemi walikabidhiwa mtoto wao wa kupanga na Mtawa Annastacia, mwaliko alimkumbatia Neema na kumwita mama na kumwahidi kuwa ataenda naye. Neema alidondokwa ana chozi la furaha na kumkambatia Mwalikio kwa mapenzi ya mama mzazi. Hili lilikuwa ni chozi la heri kwa Neema.
- Dick alimweleza Umu kuwa siku waliokutana katika uwanja wa ngege wa wakasifiri pampja, hiyo ndiyo ulikuwa siku ya heri zaidi kwake. Nasaha alizopewa na Umu zilimfunza thamani ya maisha. Jisadfa, huu ndio wakati Dick alikuwa ameamua kubadilisha maisha na kuishi maisha mapya yasiyokuwa ya kuvunja sheria.
- Mwaliko alimwambia babake kuwa kuja katika hoteli ya majaliwa kuliwatea heri kwa kuwa familia yao sasa imepanuka. Sasa amekutana na watu aliokuwa tu anasikia wakutajwa.
- Dick alitoa shukrani tele kwa elimu kwa kuwa alimpa matumaini kuwa siku moja watampata ndugu yao Mwaliko. Mwaliko hata anapomtazama Umu, macho yakiwa yamefunikikwa na vidimbwi vya machozi, anajua kuwa familia yao imerudiana japo katika mazingira tafauti.

## <u>SEHEMU B TAMTHILIA YA KIGOGO</u>

## KIGOGO

a) i) – Maneno ya Majoka
- Anamwambia Ashua
- Ofisini mwa Majoka
- Ni baada ya Ashua kumkataa Majoka
  Kimapenzi alipokwenda kutaka msaada kwake

**1 x 4 = 4**

ii) Mbinu – Swali la balagha – uliona nini kwa huyo zebe wako? (al 2 )

- Nidaa – Eti mapenzi! (al 2 )
- Kutaja alama 1
- Mfano alama 1

iii) Hulka za Majoka

- Dharau/ bezo – Eti mapenzi!
- Mpyaro – zebe ( mjinga / mpumbavu) 1 x 2 = 2

**1 x 2 = 2**

iv) **<u>Ukandamizaji wa mwanamke</u>**

- <u>kupigwa:</u> Ashua akiwa gerezani anapigwa na askari
- <u>kubezwa / kukejeliwa</u>: Tunu anakejeliwa na Ngurumo na walevi wengine
- <u>Chombo cha mapenzi</u>. Majoka anamtaka Ashuakimapenzi anapokwenda kumwomba msaada.
- Kijakazi nyumbani. Majoka anamtuma chopi kumuagiza mkewe kumpikia kuku na nyama na kumuokea chapatti
- Kutusiwa. Boza anamwambia Sudi kuwa asifikiri kuwa yeye anauza nyong'a kama Tunu wake.
- <u>Kufungwa.</u> Ashua anafungwa na Majoka
- <u>Kunyimwa kura/uongozi.</u> Nurumo anamwambia Tunu kuwa kama hampi kura Majoka ni heri ampe paka wake. Majoka lakini si mwanamke Tunu.
- <u>Kunyimwa ajira.</u> Licha ya Ashua kufuzu taaluma ya ualimu, hakuajiriwa na serikali. Anaishia kuchuuza maembe sokoni la chapakazi.
- <u>Kuozwa bila hiari.</u> Majoka nataka kumwoza Tunu kwa mwanawe Ngao Junior bila hiari yake.
- <u>Kunyimwa fidia.</u> Majoka alitaka kumnyima Hashima fidia baada ya kifo cha mumewe

**Zozote 5 x 2 = 10**

**b) Tamaa ya viongozi.**

i) <u>Tamaa ya uongozi</u>. Majoka ana tama ya.kuongoza bila upinzani toka yeyote Yule. Anaamua kumwangamiza Jabali mpinzani wake.

ii) <u>Tamaa ya kuwarithisha jamaa zao uongozi</u>. Majoka anataka kumrithisha mwanawe Ngao Junior Uongozi pude tu atakapotoka ngambo.

iii) <u>Starehe na anasa</u>. Majoka anaenda kula na kuogelea katika hoteli yake ya Majoka and Majoka modern resort.

iv) <u>Ulinzi</u>: Majoka alitaka ulinzi kutoka askari wake.

v) <u>Tamaa ya kujenga nyumba za kifahari</u>. Majoka alitamani kujenga nyumba /hoteli ya kifahari katika Soko la Chapakazi.

vi) <u>Tama ya mapenzi na wake za watu</u>. Majoka ana tamaa ya kushiriki mapenzi na Ashua mkewe Sudi.

vii) Tama ya kuoza wanao <u>wake waliosoma</u>. Majoka anataka Ngao Junior amwoe Tunu, msichana aliyesomea sheria hadi kiwango cha shahada ya uzamifu.

viii) Tamaa ya <u>kupewa sifa sufufu</u>. Majoka ni lazima atangazwe kupitia vyombo vya habari na mjumbe.

ix) Tamaa ya kuungwa mkono. Majoka anapata uungwaji mkono kupitia watu kama Ngurumo, Asiya na Boza na ambao wanapewa hongo kwa ajili – hii.

x) Tamaa ya shule zao kufunzwa na walimu waliofuzu vyuoni. Majoka anataka Ashua afunze katika shule zake kwani tayari anefuzu na kupata shahada ya elimu.

xi) Tamaa ya kupata sanamu. Majoka anataka Sudi amtengenezee sanamu itakayotumiwa katika sherehe za uhuru.

xii) Tamaa ya kupata kodi. Majoka anawatoza kodi wafanyibiashara wa soko la chapakazi kwa manufaa yake mwenyewe.

**Zozote 10 x 2 = 20**

**SEHEMU C TUMBO LISILOSHIBA**

**MWONGOZO**

4.a)

- Kauli ya kwanza ni ya mbura
- Kauli ya apili ni ya sasa.
- Walikuwa nyumbani kwa Mzee Mambo
- Mzee Mambo alikuwa ameandaa hafla ya kusherekea mtoto wake kusajiliwa kwenye shule ya nasari na wa pili meno yalikuwa yamepasua ufizi.
- Wanasema haya baada ya kula sana kwenye sherehe hiyo. **4 x 1 = 4**

b)

- Mzee Mambo kuwa waziri kivuli wa wizara zote – anapokea mshahara lakini hana kazi yoyote.
- Wafanyikazi ni watepetevu-wanafika kazini lakini hafanyi lolote pale kazini.
- Vyeo vya mzee Mmambo vinampa fursa ya kupakuwa mshahara (yeye anachota tu hapewi) uk 37.
- Mzee mambo kuandaa sherehe kubwa ambayo inaangaziwa na vyombo vya habari.
- Wizara moja inaendeshwa na mawazirir wawili – Sasa na Mbura wanadai kuwa wao ni mawaziri wa wizara ya Mipango na mipangilio.
- Sasa na Mbura kuendesha wizara kwa namna ya kujifaidi. Wanasema wizara inawaendesha hasa. Uk 37.
- Magari ya serikali kutumiwa vibaya kwenye sherehe ya Mzee Mambo kuleta jamaa zake, kuleta sherehe havipipikwi hapo bali vinaagizwa kwa mali ya umma. Uk 39.
- Mbweo anayoitoa Mbura (uk 40) ni ishara ya shibe aliyonayo. Hizi ni dalili za majitapo/kiburi cha viongozi kuridhika na hali yao ya kuendelea kufaidi kwa wizi wa mali ya uuma.
- Maelezo ya jinsi Sasa na Mbra wanafakamia chakula upsei yanatupa taswira ya jinsi wenye uwezo wanapapia mali ya umma bila kuona haya.

- Mbweo anayoitoa Mbura (uk 40) ni ishara ya shibe aliyonayo. Hizi ni dalili za majitapo/kiburi cha viongozi kuridhika na hali yao ya kuendelea kufaidi kwa wiziz wa mali ya umma.
- Matajiri hawajali lawama kutokana na wizi wao wa mali ya umma.
- DJ kwenue sherehe ya Mzee Mamabo hajali lawama kwa kulipwa mabilioni ya pea kutoka kwenye hazina ya umma.
- DJ ana duka la dawa ambalo mtaji wake ni bohari kubwa ya dawa za serikali.
- DJ na wenzake wanapaata huduma za kimsingi kama vile maji ya umeme huku raia wakiumia. **(Hoja zozote 10 x 1=10)**

c)

- Magonjwa yanayosababishwa na kula lishe isiyobora mfano sukari, presha, saratani, obesti n.k
- Kuna mauaji- watu wanauana kwa kutumia silaha za maangamizi kama vile risasi na mabomu au hata kunyongana kutokana na unyakuzi wa mali ya umma.
- Kuna hai ya kuuna kifikira na kimawazo.
- Uhalifu wa kunyang’anyana mali.
- Kutovukwa na utu/ukosefu wa heshima.
- Kutojirudi kutokana na makosa wafanyayo/kukosa kukiri na kuomba msamaha watendapo maovu.
- Kuhalalisha wizi/unyakuzi – inasemwa kuwa aliyepewa hapokonyeki (ubinafsi)

5. a)

- Tukio la kubakwa linampotesea fahamu na anaaibika sana anapozinduka na kujipata akiwa uchi uk 47
- Mwanamke kujeruhiwa – Baada ya Sara kubakwa na janadume lile, anaharibiwa na kuvuja damu.
- Mwanamke kuvunjiwa ujanajike na utu wake.
- Maisha ya mwanamke kuingiliwa na kuharibiwa.
- Masomo yake yanakatizwa – mwalimu mkuu alimkabidhii Sara barua ya kumfukuza shuleni (uk 49)
- Mwalimu mkuu hamsikilizi wala kumhurumia – badala yake aliongoza kumkejeli na kumweleza ile haikuwa shuke ya wazazi bali wa wasichana. Anasema hawafundishi wanawake hapo.
- Mwanamke anateseka kiakili – Sara anaingiwa na mawazo mengi jinsi atakvyoukabili ule ujauzito. Anafikiria hata kuitoa ile mimba, kuhama kwao na hata kujiua.
- Mwanamke katika umri mdogo anabebeshwa mimba jinsi Sara alivyofanysihwa. Mzigo huo ungekuwa na changamoto nyingi kutokana na umri wake mdogo.
- Kuishi adhabu ya wazazi – Sara anahofia babake angemchinja kwa ujauzito wake.
- Kuogopa kutoa taarifa ya kubakwa kwa wazazi kwa sababu wazazi hawangemwamini.

- Kuishi maisha ya kimaskini – msimulizi anaeleza kuwa Sara angekuniwakunjiwa matambatra yake na kuruishiwa nje.
- Kila mara mwanamke anapobakwa, anayelaumiwa ni mwanamke na hata huonwa kama shetani. Uk 48 **(hoja 10 x 1 = 10)**

b)

Mtahiniwa azingatie masharati ambayo mwanamume anafaa ayazingatie pamoja na athari zake katika maisha y andoa.)

- Dadi ndiye mchuma riziki-yeye ni muuza samaki na apatacho kinatumiwa kuilisha jamaa yake. Pesa za mkewe ni za kununua fasheni mpya mpya na mapambo.
- Dadi anasaidia kazi za nyumbani lakini mkewe Kidawa hatosheki na hayo.
- Kidawa hakubali kuwa mwanamume kazi ni za nje si za ndani na kuwa Dadi kufanya kazi za ndani ni hisani tu. Uk 60.
- Dadi analazimika kushika shughuli za upishi kama vile kukuna nazi na kutia mboga tui.
- Dadi anaosha nyumba, kufagia, kufua na hata kupiga nguo pasi.
- Wanandoa kujiwekea masharti ya uzazi. Wanahiari kumzaa mtoto mmoja tu kutokana na athari za usasa.
- Dadi hataki mkewe atembeze bidhaa za kuwauzia wateja. Kila mara mkewe anapofanya hivyo, anaumia sana. Anaiona hiyo kama fursa ya mkewe kuhusiana na wanaume wengine . Uk 61.
- Dadi anaona ugumu wa masharti ya mkewe katika maisha ya ndoa lakini anashinda kumweleza.
- Licha ya kuwa Dadi aliona ugumu wa kuzingatia masharti aliyowekewa na mkewe, hangeyavunja. Angefanya hivyo ndoa yao ingevunjika na huko kungekuwa ni kumvunja yeye pia.
- Dadi kushuku mkewe ana uhusiano wa kimapenzi na mwalimu mkuu. Hali hiyo inampa wasiwasi sana hata anashindwa kula.
- Kila mara Dadi alitarajiwa kuwa baada ya kula angeviondoa vyombo mezani na hata kuvisafisha.
- Dadi anapoamua kuzua mpango wa kupeleleza uhusiano wa mkewe na mwalimu mkuu, anafumaniwa na watu akiwa amepanda apipu na anaagnuka na kuumia vibaya sana jambo linalomshutua sana mkewe pamoja na mwalimu mkuu anayelazimika kumwitia ambulensi impeleka hospitalini

**<u>SEHEMU D</u>**

**MWONGOZO WA KUSAHIHISHA**

**<u>USHAIRI B</u>**

a) Kuonyesha madhila anayopitia mwanamke/mama mikononi mwa mwanamme.

**( 1 x 2 = alama 2)**

b) Ngonjera – ni mazungumzo kati ya Mama na Mwana.

**(aina 1, idhibati 1 jumla alama 2)**

c) Kufanywa kufua nguo

Mama huenda shambani peke yake.

Baba hubaki nyumbani tu na kupiga gomzo mitaani.

Baba hamthamini mama.

Mama hukata kuni kondeni na kuzibeba kichwani.

Mama akichelewa kufika nyumbani akitoka kondeni huadhibiwa.

Mama ndiye hutafuta chakula

**(yoyote 5 x 1= alama 5)**

d) Ubeti una mishororo sita

- Mshororo umegawika katika vipande viwili isipokuwa mshororo wa tano ambao umegawika katika kipande kimoja.
- Kila mshororo una mizani kumi na sita isipokuwa mshororo wa sita ambao una mizani tano
- Kibwagizo kimefupishwa
- Mpangilio wa vina:

li ----------------yo
li ---------------yo
li----------------yo
li ---------------yo
e
mbe------------go

**( alama 1 kwa kila jibu sahihi, jumla alama 5)**

e) Umenifanya nihisi uchungu ambao nimekuwa nao kwa miaka mingi, usidhani kuwa nayapenda madhila na mashaka, nakerwa na hali yake ya kunidhibiti kufanya jambo na sasa nichoka, ninaanaza kwa hakika kujitayarisha kwa mapambano, hilo nakwambia.

**(alama 4)**

f) (i)Jaza – malipo kwa kutenda wema **(alama 1)**

(ii) muhibu – mpenzi **(alama 1)**

**MWONGOZO**

**<u>SHAIRI A</u>**

a) - Kuwahimiza watu washikilie taalamu zao walizofuzu

- Kukashifu/ kushutumu/kukejeli ukosefu wa mwelekeo katika jinsi mambo yanavyoendeshwa.

- Kukuza msamiati wa wasomaji wake kuhusu watu wa kazi hizo.

**(malengo yoyote matatu 1 x 3 = alama 3)**

b) (i) Msuko – kibwagizo kimefupishwa

(ii) Ukara – vina vya utao vinatiririka ilhali vya ukwapi vinabadilikabadilika kutoka ubeti mmoja hadi mwingine.

**(bahari na maelezo yake alama 2 x 2 = alama 4)**

**c) <u>Inkisari</u>**

- Walojitia – waliojitia
- Kiwapi – kiko wapi
- Kalibebe - akalibebe
- Gonga – agonga
- Osha - aosha
- Kawa – kawa

**Tabdila**

- Anahiyari - anahiari
- Yamewavunda – yamewavunja

**Kuboronga sarufi/ kufinyanga sarufi**

- Muashi vyuma adunda – mwashi adunda vyuma
- Muhunzi tiba apenda – muhunzi apenda tiba
- Baharini anakwenda – anakwenda baharini nk.

**Utohozi**

- Saveya - soroveya

**Lahaja**

- Yamewavunda
- Anafundafunda

**(kutaja na kutoa mfano 1, aina tano za uhuru 1 x 5 = alama 5)**

d) Kinaya – matendo ya wahusika ni kinyume na matarajio yetu ya kazi wanazofaa kuzifanya, kwa mfano, muashi agonga vyuma ilhali jaji anagonga misumari.

**( kutaja mbinu 1, maelezo 1 = alama 2**

e) Daktari anasuka/ anasokota kamba naye saveya amakuwa stadi wa kuvunjavunja mawe. Mtunzaji hazina au mali ya taje ndiye anayetumia vibaya, ni kinyume kimetiliwa mkazo.

**(alama 4)**

f) Masikitiko – anasikitika kuwa watu wanaopaswa kufanya mambo fulani hawafanyi wanavyostahili bali wanafanya kinyume na matarajio.

Hakiki jibu la mtahiniwa)

**(kutaja 1, maelezo 1 = alama 2)**

## SEHEMU E

**MWONGOZO FASIHI SIMULIZI**

1 a) muktadha Km kilimo

b) maudhui k.v malezi, kazi n.k

c) mtindo k.m kweli kinzani

d) jukumu k.v kusifu, kukashifu,kuhimiza n.k

e) maana – maana sawa , maana zinazokinzana n.k

2. i) kweli kinzani

ii) Sitiari / tashihisi

3. Misimu ni semi za muda ambazo hubuniwa na kutumiwa katika mazingira maalum na katika kipindi maalum cha mwaka ilihali lakabu ni jina la msimbo au la kupanga ambalo mtu hujibandika ama hubandikiwa kutokana na sifa zake za kimaumbile, kitabaka, kitabia au kimatendo.

4. i) Miviga ni sherehe za kitamaduni ambazo hufanya na jamii yoyote katika kipindi maalum cha mwaka. M.f jando / harusi.

   ii) Hasara za miviga
   - baadhi zimepitwa na wakati
   - -baadahi ya mviga k.m ukeketaji wa wake hukinzana na malengo ya kitaifa.
   - Hujaza watu hofu.
   - Baadhi huhusisha ushirikana.
   - Baadhi kugahrimu kiasi kikubwa cha pesa/mali.
5. i) Malumbano ya utani.
   ii) Sanaa ya ngoma (huwasilishwa kutumia milio ya ngoma badala ya mdomo)